



Ufahamu Umoja wa Kimataifa wa Wawezeshaji – (International Association of Facilitators - IAF)

Umoja wa Kimataifa wa Wawezeshaji (International Association for Facilitators -IAF) ni umoja wa Kimataifa wa kuwezesha michakato ya wawezeshaji na kuwakilisha wawezeshaji kutoka nyanja mbali mbali zikiwemo za sekta ya maendeleo, sekta ya umma na sekta binafsi. Umoja huu ulianzishwa mwaka 1994 na hadi sasa umoja huu una wanachama zaidi ya 2,000 duniani kote. Umoja huu una sura/matawi 57 ya Asili/Kitaifa na Vikundi 7 vya wale wenye mahitaji maalum kutoka katika mabara matano duniani kote. Sura/tawi ni jamii ya wawezeshaji ambao ni wanachama IAF kutoka nchi moja ambao kwa pamoja hupanga shughuli za uwezeshaji kulingana na majukumu ya msingi ya Umoja huu na kuendelea kuhamasisha nguvu ya uwezeshaji duniani kote.

IAF Afrika

Umoja wa Wawezeshaji Sura ya Afrika kwa hivi sasa una wanachama zaidi ya 100 kutoka katika sura/matawi ya kitaifa 9 ambayo ni; Bukina Faso, Ethiopia, Kenya, Nigeria, Rwanda, Tanzania, Togo, Tunisia na Uganda. Pia kuna wanachama kutoka Africa Kusini, Algeria, Angola, Benin, Botswana, Cote d'Ivoire, Gambia, Ghana, Misri, Morocco, Mozambique, Namibia, Zambia na Zimbabwe. Wanachama hawa wanaweza kushiriki katika majadiliano katika mtandao na pia kushiriki katika shughuli nyingine kama vile:-

- Juma la uwezeshaji Kimataifa – Hii hufanyika kusherekea taaluma ya uwezeshaji inayofanyika mwezi Oktoba kila mwaka
- Tuzo za matokeo ya uwezeshaji – Hili ni tukio la kimataifa la kutambua matokeo ya bora katika taaluma ya uwezeshaji
- Program ya Kuthibitisha taaluma ya uwezeshaji – Hii ni program ya kupima na kutambua uwezo wa wawezeshaji na kuwapa vyeti vya uthibitisho (thibati)
- Kuendeleza shughuli za sura/tawi kitaifa katika uwezeshaji pamoja na kukuza na kuhamasisha utaaluma ya uwezeshaji

Wanachama wanahimizwa kuanzisha sura/matawi katika maeneo yao na jamii ili kuhamasisha na kujiendeleza wenyewe katika taaluma ya uwezeshaji kwa ujumla.

Kwa nini ujiunge na IAF

- 1) **Unatuhitaji.** Pamoja na wewe, Wanachama wa IAF hufanya kazi na vikundi, kwa kusaidia katika kutimiza malengo ya kuleta mabadiliko chanya duniani. IAF inatambua changamoto unazokumbana nazo katika kuanzisha matumizi ya mbinu au michakato shirikishi katika kupanga na kuwezesha vikundi kwa na malengo jumuishi zaidi, kuongeza ushiriano na ufanisi. Kuendelea kusaidia mafunzo endelevu na kukuza taaluma ambavyo ni ufunguo katika kudumu na kustawi kama mwezeshaji na kukuza taaluma.
- 2) **Tunakuhitaji.** Kama umoja wa wanachama, tunahitaji kuongeza sauti za ushiriki kwa wingi iwezekananvyo katika mazungumzo ya kimataifa kuhusu umuhimu wa uwezeshaji kwa vikundi na mashirika duniani kote. IAF inilisherehekea miaka 20 ya kuanzishwa kwake mwaka 2014 na hivi sasa imejikita katika hatua ya kukua. Uanachama wako unasaidia umoja kufikia watu wengi na kuupatia nguvu katika mtandao wa kimataifa.
- 3) **Dunia inahitaji wawezeshaji mahiri.** Tazama kote. Katika kila ngazi ya jamii, kila nchi, kila bara, vikundi vinatafuta njia mbali mbali za kutatua masuala magumu, kusuluhisha migogoro ya ndani na kufanya maamuzi sahihi kwa pamoja. Viongozi, wameendelea kutambua umuhimu wa kukuza mashirikiano na kuchangia katika majukumu ya uwajibikaji wa pamoja. Wawezeshaji wenye ujuzi mahiri wanajaza nafasi muhimu katika kuwezesha kuleta mabadiliko chanya.

Kwa taarifa zaidi tembelea tovuti ya IAF : www.iaf-world.org

**Kwa taarifa zaidi kwa kanda ya Afrika tembelea: <https://www.iaf-world.org/site/regions/africa>
Au wasiliana na Benjamin Manu (Mratibu wa Kanda ya Africa) rep.africa@iaf-world.org**